

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA A**

**689**

**VITENDO VYA KUJIFUNZA SAYANSI**

**Muda: Saa 3**

**Mwaka : 2021**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



2

## **SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Ainisha maeneo manne ya mwili ambayo mwanafunzi wa Elimu ya Awali anapaswa kujifunza kuyafanyia usafi.
2. (a) Taja mambo manne yanayoathiri usalama wa wanafunzi wa Elimu ya Awali katika mazingira ya shule.  
(b) Orodhesha aina nne za majanga ya asili.
3. Tofautisha istilahi ‘tathmini ya mwanafunzi’ na ‘tathmini ya mwalimu’ kama zinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji.
4. Ni kwa vipi utamfundisha mwanafunzi wa Elimu ya Awali kufua nguo? Bainisha hatua nne.
5. (a) Tofautisha mbinu ya bungua bongo na mbinu ya maswali na majibu kama zinavyotumika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.  
(b) Taja faida mbili za kufundisha kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu kwa wanafunzi wa Elimu ya Awali.
6. Bainisha vifaa vinne vinavyotumiwa na wanafunzi wa Elimu ya Awali katika kufanya usafi wa mazingira na onesha kazi ya kila kifaa.
7. Kwa nini ni muhimu kufanya uchunguzi wa kisayansi katika mazingira tunayoishi? Toa hoja nne.
8. (a) Ni kwa namna gani utatofautisha magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza?  
(b) Je, ni magonjwa gani mtoto anaweza kupata kwa kurithi kutoka kwenye familia yake? Taja magonjwa manne.
9. Bainisha namna nne za kuandaa na kuhifadhi chakula safi na salama kwa matumizi ya watoto.
10. Eleza dalili nne za kila ugonjwa katika magonjwa yafuatayo:  
(a) Nyongea  
(b) Unyafuzi

### **SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. (a) Mwanafunzi wa Elimu ya Awali anapaswa kupatiwa virutubisho mbalimbali vinavyounda mlo kamili ili kuimarishe afya yake. Thibitisha kauli hii kwa kutumia mifano mitano.  
(b) Ni kwa namna gani virutubisho vinavyounda mlo kamili huathiri afya ya mtoto vikitumiwa kwa wingi kupita kiasi? Toa mifano mitatu.
12. (a) Fafanua kuhusu njia za maambukizi, dalili na namna ya kujikinga na ugonjwa wa dengue.  
(b) Je, ni athari zippi humpata mwanafunzi wa Elimu ya Awali anayecugua mara kwa mara? Bainisha athari nne.
13. (a) Eleza majanga matano yanayoweza kutokea kwenye mazingira tunayoishi na jinsi ya kukabiliana nayo.  
(b) Bainisha namna shughuli za ukataji miti, viwanda na uchimbaji madini zinavyochangia uchafuzi wa vyanzo vyaa maji.

### **SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

14. (a) Kwa kutoa hoja tatu, eleza umuhimu wa andalio la somo kwa mwalimu wa Elimu ya Awali.  
(b) Andaa mfano wa andalio la somo kuhusu ‘Faida za Kula Chakula Bora.’
15. (a) Somo la Vitendo vya Kujifunza Sayansi lina umuhimu gani kwa wanafunzi wa Elimu ya Awali? Eleza faida tatu.  
(b) Eleza misingi sita ambayo mwalimu anapaswa kuzingatia katika kumfundisha mwanafunzi wa Elimu ya Awali.
16. (a) Kwanini mwalimu anapaswa kuandaa Azimio la Kazi na kulitumia? Eleza sababu tatu.  
(b) Wakati wa kuandaa Azimio la Kazi ni mambo yapi muhimu mwalimu anapaswa kuyazingatia? Ainisha mambo manne.